

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 67 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** SEPTEMBER 2026

SAFARI YA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU: KUTOKA UTS KUELEKEA DIRA YA 2050



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke (kulia) na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania  [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

TUMPE USHIRIKIANO MAKAMU WA RAIS NDEJEMBI, TUSIMAMIE WAJIBU WETU KWA MAENDELEO YA ELIMU

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inampongeza kwa dhati Mhe. Deogratius John Pancras Ndejembu kwa kuapishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume inamtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake mapya ya kitaifa na inaamini kuwa uongozi wake utaendelea kutoa mchango muhimu katika kutekeleza ajenda za Serikali na kuharakisha maendeleo ya Taifa.

Nafasi ya Makamu wa Rais ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali na kusimamia maeneo mbalimbali ya maendeleo ya Taifa. Kwa kutambua umuhimu huo, TSC inaahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa Mhe. Ndejembu na Serikali kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yanayohusu usimamizi wa utumishi wa walimu. Tume itaendelea kutekeleza wajibu wake kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo, huku ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha sekta ya elimu inaendelea kuimarika.

Pamoja na jitihada za Serikali katika kuboresha elimu, mafanikio ya sekta hiyo hayawezi kufikiwa bila walimu kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Mwalimu ndiye mhimili wa utekelezaji wa elimu darasani na ana nafasi kubwa katika kujenga maarifa, ujuzi na maadili kwa kizazi cha sasa na kijacho. Kwa msingi

huo, TSC inatoa wito kwa walimu wote nchini kuongeza uwajibikaji, weledi, uadilifu na kujituma katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Tume inawakumbusha walimu kuwa utekelezaji wa wajibu wao hauishii kufika kazini na kufundisha pekee, bali unahusisha kuzingatia maadili ya kazi ya Ualimu, kutunza muda, kuandaa na kufundisha masomo kwa ufanisi, kuwalea wanafunzi kwa misingi ya maadili na kushiriki kikamilifu katika shughuli zinazolenga kuboresha mazingira ya ujifunzaji. Nidhamu na uwajibikaji wa mwalimu ni sehemu ya msingi ya kuhakikisha uwekezaji unaofanywa na Serikali katika sekta ya elimu unazaa matokeo yanayotarajiwa.

TSC inaendelea kumpungeza Mhe. Deogratius John Pancras Ndejembu kwa kushika wadhifa huo muhimu na inamhakikishia ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya Taifa. Wakati Serikali ikiendelea kuweka mazingira bora ya utoaji wa elimu, ni wajibu wa kila mwalimu kutumia fursa hiyo kwa kutekeleza majukumu yake kwa uaminifu na weledi. Tumpe ushirikiano Makamu wa Rais Ndejembu, tushirikiane na Serikali, na zaidi ya yote tusimamie wajibu wetu ili kwa pamoja tuijenge sekta ya elimu yenye ubora na inayochochea maendeleo ya Taifa.

KATUNI

TUNAKUPONGEZA
MHE. DEOGRATIUS NDEJEMBI
NA TUNA AHIDI KUKUPA USHIRIKIANO
KWA MAENDELEO YA ELIMU



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgenders
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 756 927 131 & +255 735-255238 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz

Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

SAFARI YA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU: KUTOKA UTS KUELEKEA DIRA YA 2050

Na Mwandishi Wetu

Mwaka 2026 ni mwaka wa kipekee katika historia ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kwani ni mwaka ambao Tume inatimiza miaka 10 tangu kuanza rasmi kutekeleza majukumu yake katika mfumo wa sasa. Miaka 10 ni kipindi kinachotoa fursa siyo tu ya kutazama Tume ilikotoka, bali pia kutafakari kwa kina safari ya usimamizi wa utumishi wa walimu nchini, mabadiliko yaliyofanyika, sababu za mabadiliko hayo na mwelekeo wa safari inayofuata. Kwa kuzingatia kwamba Tanzania imeanza rasmi kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kumbukizi hii inapata maana zaidi kwa sababu mustakabali wa elimu na wa mwalimu ni sehemu muhimu ya mustakabali wa Taifa.

TULIPOTOKA: KUTOKA UTS HADITSC

Historia ya TSC ya sasa haiwezi kutenganishwa na historia ndefu ya namna Tanzania ilivyokuwa ikisimamia utumishi wa walimu. Mara baada ya Uhuru wa Tanzania Bara (Tanganyika), Serikali ilichukua hatua ya kuunganisha utumishi wa walimu wa umma na wa sekta binafsi chini ya Sheria Na. 6 ya mwaka 1962 ya Huduma kwa Walimu (*Unified Teaching Service – UTS*).

UTS ilishughulikia masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu wa Serikali na waajiri wengine, ikiwemo ajira, kuthibitishwa kazini, kupandishwa vyeo, pamoja na maadili na nidhamu. Mwalimu aliyeajiriwa na mwajiri mwingine nje ya Serikali alijaza mkataba na mwajiri wake na kuuwasilisha UTS kwa ajili ya kusajiliwa na kupewa namba ya usajili (*UTS No.*). Mapendekezo ya kuthibitishwa kazini na kupandishwa cheo yaliwasilishwa UTS, na waajiri walitekeleza maamuzi yaliyotolewa na chombo hicho.

Katika kipindi hicho, misingi ya maadili ya kazi ya Ualimu iliandaliwa na kufundishwa katika Vyuo vya Ualimu, huku kila mwalimu akitakiwa kuzingatia misingi hiyo bila kujali aina ya mwajiri wake.



Mwenyekiti wa Kwanza wa TSC Bw. Oliva Joseph Mhaiki

Hata hivyo, kadiri idadi ya walimu na mahitaji ya walimu yalivyoongezeka, ndivyo changamoto za mfumo wa usimamizi wa utumishi wao zilivyojitokeza zaidi.

KWA NINI MFUMO ULIENDELEA KUBADILIKA?

Taarifa ya Tume ya Rais ya Elimu ya mwaka 1980–1982, iliyoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jackson Makweta, ilibaini changamoto katika usimamizi wa utumishi wa walimu.

Tume hiyo ilibaini udhaifu katika mfumo wa usimamizi wa Huduma kwa Walimu (UTS), uliokuwa chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kadiri

idadi ya walimu ilivyoongezeka, changamoto za kuwapatia huduma stahiki nazo ziliongezeka.

UTS ilikuwa ikifanya kazi kama kitengo ndani ya iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, huku usimamizi wa walimu ukiihusisha pia Ofisi za Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mikoa na Wilaya. Kwa kuzingatia ongezeko la walimu na changamoto zilizokuwepo, ilionekana kuwa mfumo huo ulihitaji maboresho ili uweze kukidhi mahitaji mapya ya usimamizi wa utumishi wa walimu.

TSC YA MWAKA 1989: HATUA YA KWENDA KWENYE MFUMO MAALUMU

Kufuatia mabadiliko hayo, Sheria Na. 1 ya mwaka 1989 ilianzisha

SAFARI YA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU: KUTOKA UTS KUELEKEA DIRA YA 2050

Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers' Service Commission – TSC*), ambayo wakati huo ilikuwa Idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na UTS yalihamishiwa kwenye Tume hiyo. Hatua hiyo ilikuwa ishara ya kutambua upekee wa taaluma ya Ualimu na umuhimu wa kuwa na mfumo maalumu wa kusimamia utumishi wa walimu.

Hata hivyo, mabadiliko ya mfumo wa Utumishi wa Umma yaliendelea. Mwaka 2002, kupitia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka huo, Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 1 ya mwaka 1989 ilifutwa na Tume ikawekwa chini ya Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) kama Idara ya Utumishi wa Walimu.

Idarahiyoiliendeleakushughulikia masuala ya utumishi wa walimu, lakini mfumo huo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo upungufu wa rasilimali watu na fedha pamoja na changamoto katika kushughulikia rufaa za walimu dhidi ya maamuzi yaliyotolewa.

Kutokana na wingi wa walimu, upekee wa majukumu yao na umuhimu wa taaluma ya Ualimu katika maendeleo ya Taifa, hitaji la kuwa na chombo maalumu cha kusimamia utumishi wa walimu liliendelea kuwa muhimu.

KUANZISHWA TENA KWA TSC

Hatua hiyo ilisababisha Serikali kuwasilisha Bungeni Muswada wa kuanzisha Tume ya Utumishi wa Walimu. Hatimaye, Tume ya Utumishi wa Walimu ilianzishwa kupitia Sheria Na. 25 ya mwaka 2015.

Chini ya Kifungu cha 5 cha Sheria hiyo, Tume imepewa jukumu la kusimamia masuala ya utumishi wa walimu, ikiwemo maadili na nidhamu ya walimu walio katika utumishi wa umma.

Mwaka 2016 ukawa mwanzo wa safari ya Tume ya sasa ya kutekeleza majukumu hayo katika mfumo mpya. Tangu wakati huo, TSC imekuwa sehemu muhimu ya mfumo wa Serikali katika kusimamia utumishi wa walimu na kuhakikisha kuwa taaluma hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, maadili na



Mwenyekiti wa Pili wa TSC, Prof. Willy Komba

viwango vinavyotakiwa.

MIAKA 10: KUTOKA USIMAMIZI WA UTUMISHI HADI KUJENGA UWAZI NA UWAJIBIKAJI

Miaka 10 ya TSC ya sasa haiwezi kupimwa kwa idadi pekee ya walimu walioajiriwa, waliopandishwa vyeo au mashauri yaliyoshughulikiwa. Maana kubwa ya kipindi hiki ipo pia katika mabadiliko ya namna ambavyo utumishi wa walimu unasimamiwa.

Katika kipindi hiki, msisitizo wa Tume umeendelea kuwa katika kujenga mfumo unaotambua kuwa usimamizi wa utumishi wa walimu siyo suala la ajira na nidhamu pekee, bali ni sehemu ya kujenga mazingira ambayo mwalimu anaweza kutekeleza wajibu wake kwa weledi,

uwajibikaji na ufanisi.

Hii imehusisha kuendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma, matumizi ya teknolojia katika usimamizi wa utumishi, kuimarisha taratibu za kushughulikia changamoto za walimu, kusimamia maadili na nidhamu, pamoja na kuendeleza mazingira ya haki na uwajibikaji katika utumishi.

Mabadiliko haya yanaonesha kwamba TSC haiwezi kubaki kuwa taasisi inayosubiri changamoto zitokee na kuzishughulikia. TSC ya sasa na ya baadaye inahitaji kuwa taasisi inayotazama mbele, inayotambua mabadiliko yanayotokea katika elimu, teknolojia na mazingira ya kazi, na kujiandaa mapema kuyakabili.

Mwalimu siyo mtumishi

SAFARI YA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU: KUTOKA UTS KUELEKEA DIRA YA 2050

anayetekeleza majukumu ya kawaida ya Serikali. Kazi yake ina athari ya moja kwa moja katika aina ya kizazi kinachojengwa na Taifa. Maarifa, ujuzi, maadili, ubunifu na uwezo wa kufikiri unaojengwa kwa mwanafunzi leo utakuwa sehemu ya nguvu kazi na uongozi wa Tanzania kesho.

Kwa mantiki hiyo, masuala ya ajira, maendeleo ya taaluma, maadili, nidhamu, uwajibikaji na ustawi wa mwalimu yanapaswa kuonekana ndani ya picha kubwa zaidi ya maendeleo ya Taifa.

Hapa ndipo nafasi ya TSC inapokuwa ya kimkakati zaidi: kusimamia utumishi wa mwalimu kwa namna inayoweza mwalimu kutekeleza jukumu lake la kujenga rasilimali watu ya Taifa.

TSC NA DIRA YA 2050

Tanzania sasa imeingia katika hatua mpya ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo inaweka msisitizo katika kujenga Taifa lenye ustawi, uchumi unaotegemea maarifa na teknolojia, pamoja na rasilimali watu yenye uwezo wa kushindana katika mazingira ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Dira pia inaonesha umuhimu wa kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi, inayobadilika kulingana na mahitaji ya wakati, inayotumia teknolojia, yenye ubunifu na inayojifunza maisha yote.

Kwa TSC, utekelezaji wa Dira 2050 una maana ya moja kwa moja. Taifa haliwezi kujenga rasilimali watu yenye uwezo mkubwa bila kuwa na walimu wenye uwezo wa kuandaa rasilimali hiyo.

Dira 2050 inalenga mfumo wa elimu unaokidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa na mazingira ya dunia yanayobadilika. Inasisitiza elimu inayojenga uwezo wa kufikiri kwa kina, kutatua matatizo, ubunifu, ujuzi wa kiteknolojia, ujuzi wa kidijitali, ujasiriamali na kujifunza endelevu.

Kwa hiyo, kwa upande wa TSC, safari ya kuelekea 2050 haiwezi kuwa tu kuhusu kuongeza ufanisi wa michakato ya kiutawala. Ni kuhusu kuhakikisha kuwa mfumo wa usimamizi wa utumishi wa walimu



Katibu wa Kwanza wa TSC, hayati Mwl. Winifrida Rutaindurwa

unaendana na aina ya mwalimu anayehitajika katika Tanzania ya 2050.

TSC KUELEKEA 2050

TSC ya kuelekea 2050 inapaswa kuwa Tume inayoweza kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya elimu. Hii maana yake ni kuwa mifumo ya huduma za utumishi inapaswa kuendelea kuwa ya kidijitali, rahisi, yenye uwazi na inayotumia taarifa sahihi katika kufanya maamuzi.

TSC ya 2050 inahitaji kusimamia utumishi kwa mtazamo unaomtambua mwalimu kama mtaalamu anayehitaji kuendelezwa kitaaluma, kuhamasishwa, kuwajibishwa na pia kuwezesha kufanya kazi yake kwa ufanisi.

Dira 2050 inaonesha kuwa nguvu

kazi ya baadaye itahitaji ujuzi wa kiteknolojia, uwezo wa kubadilika, ujuzi wa data, uwezo wa kushirikiana na wengine, uadilifu, ubunifu na utayari wa kujifunza maisha yote.

Tanzania ya 2050 haitahitaji watu wenye ujuzi pekee; itahitaji watu wenye uadilifu, uwajibikaji, uzalendo na uwezo wa kutumia maarifa yao kwa manufaa ya jamii.

Kwa hiyo, usimamizi wa maadili na nidhamu ya walimu siyo jukumu la kinidhamu pekee. Ni sehemu ya maandalizi ya Taifa la baadaye.

Mwalimu anayezingatia muda, anayewajibika, anayeheshimu taaluma yake, anayemlea mwanafunzi kwa maadili na anayetekeleza kazi yake kwa uadilifu anashiriki moja kwa moja katika kujenga Tanzania tunayoitaka mwaka 2050.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFTI NA ELIMU KWA UMMA TSC YAPONGEZA USIMAMIZI WA PEPMIS



Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya TSC ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa (katikati) akiongoza kikao cha Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika tarehe 13 Agosti, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Dodoma.

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeipongeza Menejimenti ya Tume kwa usimamizi mzuri wa mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS), huku ikisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu matumizi sahihi ya mfumo huo.

Kamati hiyo imeeleza hayo, Agosti 13, 2026, wakati wa kikao chake kilichofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Dodoma, kikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Bi. Mgongolwa ameipongeza Menejimenti ya Tume kwa namna inavyosimamia utekelezaji wa PEPMIS, alisisitiza kuwa mfumo huo ni nyanzo muhimu katika kuhakikisha watumishi wanapanga, kutekeleza na kutathmini majukumu yao kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa.

Amesisitiza kuwa pamoja na hatua zilizochukuliwa katika kusimamia utekelezaji wa PEPMIS, Tume inapaswa kuendelea kutoa

elimu na uelewa kwa watumishi wake katika ngazi zote ili kila mtumishi awe na uelewa wa wajibu wake na kuhakikisha taarifa za utendaji zinaingizwa kwa usahihi na kwa wakati.



Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya TSC ambaye pia ni Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa (katikati) akizungumza wakati wa kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika leo Agosti 13, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Dodoma.

“Ni muhimu kuhakikisha kila mtumishi anaelewa wajibu wake katika matumizi ya PEPMIS na anajaza taarifa zinazohitajika kwa usahihi. Hii itasaidia mfumo kutoa taswira halisi ya utendaji kazi na kuwezesha Tume kufanya tathmini na maboresho kwa wakati,” alisema Bi. Mgongolwa.

Aidha, Mwenyekiti huyo amesisitiza umuhimu wa viongozi na wasimamizi katika ngazi mbalimbali kuendelea kuwasaidia watumishi kuelewa mchakato wa upimaji wa utendaji kazi, ikiwemo upangaji wa malengo, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya utendaji.

Katika kikao hicho, Kamati ilipitia masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa majukumu ya Tume, ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha mipango, mikakati na maamuzi ya Tume yanatekelezwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia misingi ya uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali.

Kikao hicho pia ni sehemu ya maandalizi ya masuala yatakayowasilishwa katika Mkutano wa Tume kwa ajili ya kujadiliwa na kufanyiwa maamuzi kwa lengo la kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma kwa walimu nchini.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFITI NA ELIMU KWA UMMA TSC YAPONGEZA USIMAMIZI WA PEPMIS



Katibu wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ambaye pia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa taarifa wakati wa kikao cha kamati hiyo kilichofanyika tarehe 13 Agosti, 2026 katika ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFITI NA ELIMU KWA UMMA TSC YAPONGEZA USIMAMIZI WA PEPMIS



Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Aggrey Mleli (kulia) akizungumza wakati wa kikao cha Kamati hiyo kilichofanyika tarehe 13 Agosti, 2026 Katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.



Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya TSC wakiwa katika kikao kilichofanyika Agosti 13, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Dodoma.

KAMATI YA UTAWALA, FEDHA, UTAFITI NA ELIMU KWA UMMA TSC YAPONGEZA USIMAMIZI WA PEPMIS



Wajumbe wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya TSC wakiwa katika kikao kilichofanyika Agosti 13, 2026 katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Dodoma.

WATUMISHI WA TSC KIBITI WAFURAHIA HUDUMA KUSOGEZWA KARIBU



Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kibiti, Bw. Ally Masoudi, akiwa ofisini Kibiti akielezea mafanikio ya TSC katika kipindi cha miaka 10.

Na Mwandishi Wetu – Kibiti

Wakati Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ikiendelea kuadhimisha miaka 10 tangu kuanza kufanya kazi kwa mfumo mpya mwaka 2016, watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti, Mkoa wa Pwani, wameeleza kufurahishwa na kuanzishwa kwa Ofisi ya Tume ndani ya wilaya hiyo, wakisema hatua hiyo imesaidia kusogeza huduma karibu na walimu na kupunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili katika kupata huduma za kiutumishi.

Wilaya ya Kibiti ilianzishwa rasmi tarehe 1 Julai 2016, na Ofisi ya TSC Wilaya ya Kibiti ilianzishwa mwaka 2017. Kabla ya kuanzishwa kwa ofisi hiyo, walimu wilayani Kibiti walipata huduma kupitia Ofisi ya TSC Wilaya ya Rufiji ambayo ipo umbali wa takribani kilomita 85 kutoka zilipo Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

Akieleza kuhusu mabadiliko hayo, Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kibiti, Bw. Ally Masoudi, alisema kuanzishwa kwa ofisi hiyo ni miongoni mwa mafanikio yanayoonyesha namna Tume ilivyoboresha utoaji wa huduma kwa walimu katika kipindi cha miaka 10.

“Uwepo wa Ofisi ya TSC ndani ya Wilaya ya Kibiti umesaidia sana kutatua changamoto za walimu, hususan katika masuala ya upandishaji wa madaraja, ubadilishaji wa vyeo na kazi, pamoja na madai mbalimbali ya mishahara na yasiyo ya mishahara,” alisema.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa ofisi hiyo, baadhi ya walimu walilazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma, jambo lililosababisha usumbufu na wakati mwingine kuchelewesha upatikanaji wa huduma.

Kwa mujibu wa Bw. Masoudi, baada ya kuanzishwa kwa Ofisi ya TSC Kibiti

mwaka 2017, Tume iliweza kuwafikia walimu kwa karibu zaidi na kutambua changamoto zao na kuzifanyia kazi.

Alitoa mfano wa mwaka 2024, ambapo walimu 196 waliokuwa na changamoto za muda mrefu za kupandishwa vyeo walipandishwa vyeo kwa mserekeo.

MUUNDO WA TSC WAONGEZA MORALI YA WATUMISHI

Akizungumzia mafanikio mengine katika kipindi hicho, Bw. Masoudi alisema kuanzishwa kwa muundo wa TSC wenye Scheme of Service kwa watumishi wa Tume ni hatua muhimu iliyoongeza ari na hamasa ya watumishi katika kutekeleza majukumu yao.

Alisema suala hilo lilikuwa miongoni mwa changamoto zilizodumu kwa muda mrefu tangu enzi za Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD), hali iliyowafanya baadhi ya watumishi kukata tamaa na kuona kuwa huenda lisingepata ufumbuzi.

“Kwa hakika tunatoa pongezi zetu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa hatua hii. Watumishi wa TSC kwa sasa wanafuraha na ari kubwa ya kutoa huduma bora kwa walimu,” alisema.

TSCMIS YARAHISISHA HUDUMA KWA WALIMU

Bw. Masoudi pia alitaja kuanzishwa kwa Mfumo wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kuwa ni hatua nyingine muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma.

Alisema mfumo huo umesaidia kurahisisha huduma mbalimbali kwa walimu, ikiwemo usajili, upatikanaji wa mikataba ya ajira, barua za ajira na namba za utambulisho za TSC.

Alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023 hadi 2026, jumla ya walimu 195 walisajiliwa na kupata huduma hizo kwa muda mfupi.

Aidha, alisema TSCMIS imewezesha kuboresha uendeshaji wa mashauri ya kinidhamu kwa walimu, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo mchakato huo uliweza kuchukua muda mrefu.

“Tangu kuanza kwa mfumo huo mwaka 2023, Wilaya ya Kibiti imefanikiwa kusajili mashauri 28 ya kinidhamu na kufanyiwa maamuzi,” alisema.

WATUMISHI WA TSC KIBITI WAFURAHIA HUDUMA KUSOGEZWA KARIBU



Mwalimu Tatu Kassim Ally, wa Shule ya Sekondari Kibiti, akielezea namna uwepo wa TSC ulivyosaidia kuboresha huduma kwa walimu katika kipindi cha miaka 10.

HUDUMA KARIBU

Kwa upande wake, Mwalimu Tatu Kassim Ally, wa Shule ya Sekondari Kibiti iliyopo Kata ya Mtawanya, alisema kuanzishwa kwa Ofisi ya TSC Wilaya ya Kibiti kumekuwa na umuhimu mkubwa kwa walimu kwa sababu huduma zimeletwa karibu na maeneo yao ya kazi.

Alisema hapo awali walimu walilazimika kusafiri umbali mrefu, wakati mwingine zaidi ya kilomita 85, kulingana na eneo walilotoka, ili kufuata huduma za TSC.

"Huduma zimesogezwa karibu na walimu. Hili lilikuwa kero kubwa kwa sababu tulilazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma," alisema.

Mwalimu Tatu pia alisema mabadiliko katika usimamizi wa utumishi wa walimu yameongeza matumaini na ari ya kufanya kazi, hususan katika masuala ya kupandishwa madaraja na upatikanaji wa stahili.

Alisema hapo awali baadhi ya walimu walikaa muda mrefu katika daraja moja bila kupandishwa, jambo lililoweza kuathiri morali ya kazi.

MAFUNZO ELEKEZI YAONGEZA UELEWA WA WALIMU

Naye Mwalimu Hamdani J. Kisoma, wa Shule ya Msingi Ruaruke, Kata ya Ruaruke, alisema ziara za mara kwa mara zinazofanywa na watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya zimekuwa na mchango katika kuongeza uelewa wa walimu kuhusu sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utumishi.

Alisema elimu hiyo imewasaidia walimu kufahamu wajibu wao na hivyo kupunguza uwezekano wa kuingia katika makosa yanayoweza kusababisha mashauri ya kinidhamu.

"Ziara hizi zimetusaidia sana kukumbushwa sheria, kanuni, miongozo na taratibu za kufuata katika utumishi wa walimu. Hii imetusaidia kuongeza uelewa na kuepuka kuingia katika makosa na mashauri ya kinidhamu," alisema.

Mwalimu Hamdani pia alieleza kuwa mafunzo elekezi yanayotolewa kwa walimu wapya yamekuwa msingi muhimu katika kuwaandaa walimu kutekeleza majukumu yao kwa uelewa wa kutosha.

Alisema mafunzo hayo huwasaidia walimu wapya kufahamu haki na

wajibu wao kwa mujibu wa sheria na taratibu za utumishi.

KIBITI YAONESHA MAANA YA HUDUMA KUSOGEZWA KARIBU

Akihitimisha, Bw. Masoudi alisema TSC Wilaya ya Kibiti ina mafanikio mengi ya kujivunia katika kipindi cha miaka 10, huku akisisitiza kuwa mafanikio yaliyotajwa ni sehemu tu ya mabadiliko yaliyofanyika katika kuboresha usimamizi wa utumishi wa walimu.

Kwa ujumla, uzoefu wa Kibiti unaonyesha kuwa mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 hayaishii katika kuanzishwa kwa mifumo na ofisi pekee, bali yanaonekana katika kusogeza huduma karibu na walimu, kuboresha mifumo ya utoaji huduma, kuongeza uelewa wa walimu kuhusu wajibu wao na kujenga mazingira yanayoweza walimu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

"Shukrani za pekee ziende kwa Menejimenti ya TSC, watumishi wote wa TSC Makao Makuu wakiongozwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Mbena Nkwama, kwa kuiongoza TSC katika kuyapata mafanikio haya makubwa na ya kukumbukwa katika kuwahudumia walimu na kusaidia kufikia matarajio yao katika Utumishi wa Umma," alisema.



Mwalimu Hamdani J. Kisoma, wa Shule ya Msingi Ruaruke, akielezea mchango wa TSC katika kuboresha uelewa wa walimu kuhusu sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utumishi.

WATUMISHI WA TSC KIBITI WAFURAHIA HUDUMA KUSOGEZWA KARIBU



Watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti wakiwa katika picha ya pamoja na walimu nje ya jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.



Bi. Adelina Beatus Nyoni, Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu TSC Wilaya ya Kibiti, akikabidhi mipira kwa wanafunzi wenye changamoto mbalimbali za ulemavu katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika katika Shule ya Kitundu.

WATUMISHI WA TSC KIBITI WAFURAHIA HUDUMA KUSOGEZWA KARIBU



Walimu wapya wa Ajira wakiwa katika mafunzo elekezi yanayotolewa na TSC katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

WATUMISHI WA TSC KIBITI WAFURAHIA HUDUMA KUSOGEZWA KARIBU



Bi. Adelina Beatus Nyoni, Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu TSC Wilaya ya Kibiti, akikabidhi mipira kwa wanafunzi wenye changamoto mbalimbali za ulemavu katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika katika Shule ya Kitundu.

TSC YASIKILIZA NA KUAMUA RUFAA 49 ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imesikiliza na kuamua jumla ya rufaa 49 zilizowasilishwa na walimu waliopinga maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka za Nidhamu katika ngazi ya wilaya.

Taarifa hiyo imetolewa hivi karibuni na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, wakati wa majumuisho ya mkutano wa siku tano wa Tume uliofanyika jijini Dodoma.

Akifafanua kuhusu maamuzi yaliyofikiwa, Mwl. Paulina alisema kati ya rufaa 49 zilizopitiwa, rufaa 17 zilikataliwa baada ya kubainika kuwa ziliwasilishwa nje ya muda uliowekwa kwa mujibu wa sheria wa siku 45 tangu mwalimu kupokea uamuzi wa shauri lake.

Aidha, rufaa tisa (9) zilirejeshwa katika Mamlaka za Nidhamu za wilaya husika ili mashauri hayo yaanze upya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu, baada ya kubainika kuwepo kwa dosari katika mwenendo wa ushughulikiaji mashauri hayo.

Kwa upande mwingine, rufaa 12 zilikubaliwa, ambapo Tume ilitengua maamuzi yaliyotolewa na Kamati za Wilaya za Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo.

Katika rufaa 10, Tume ilikubaliana na maamuzi yaliyotolewa na Kamati hizo na kuthibitisha adhabu zilizokuwa zimetolewa. Rufaa moja (1) haikuhitimishwa ili ufuatiliaji wa kina ufanyike kabla ya kutolewa uamuzi.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Mruke, akiongoza mkutano wa Tume hivi karibuni jijini Dodoma.

Mwl. Paulina alisema Tume itaendelea kushirikiana na mamlaka za shule na wadau wengine katika kukabiliana na changamoto za kinidhamu na kudhibiti vitendo vinavyoweza kusababisha walimu kuingia katika mashauri ya kinidhamu.

Aliongeza kuwa Menejimenti ya Tume, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili na miiko ya taaluma ya ualimu ili kulinda hadhi ya taaluma hiyo.

Maboresho ya Kamati za Wilaya

Aidha, Mwl. Paulina alisema Tume imepokea na kupitia mapendekezo ya maboresho ya uteuzi wa wenyevidi na wajumbe wa Kamati za Wilaya.

Alisema katika kipindi cha kuanzia mwezi Mei hadi Agosti

2026, Sekretarieti ya Tume ilipokea mapendekezo ya kuteuliwa kwa wenyevidi na wajumbe wapya baada ya baadhi ya walioteuliwa awali kupoteza sifa za kuendelea na nafasi hizo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kuhama, kufariki na kupangiwa majukumu mengine.

Alisema mapendekezo hayo yamelenga kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika Kamati za Wilaya za Dodoma, Butiama, Mbarali, Nyasa, Rombo, Kibondo, Chemba, Njombe, Kilolo, Nkasi, Mkinga, Nzega, Mvomero, Tunduru na Mkalama.

Kwa mujibu wa Mwl. Paulina, waliopoteza sifa za kuendelea na nafasi hizo ni wenyevidi watatu (3), wajumbe wa sekondari watano (5), wajumbe wa msingi watatu (3), Maafisa Elimu wanane (8) na Makatibu Tawala wa wilaya watatu (3).

Tume yapitisha taarifa mbalimbali

Wakati huo huo, wajumbe wa Tume walipokea na kupitisha taarifa za Kamati ya Tume ya Maadili na Nidhamu ya Walimu, Kamati ya Tume ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, pamoja na Kamati ya Tume ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma.

Mkutano huo pia ulipitia na kupitisha taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka wa fedha 2026/27, pamoja na maelezo ya utekelezaji wa kazi na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2025/26 kwa Idara na Vitengo vya Tume ya Utumishi wa Walimu.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Mruke, akiongoza sala kabla ya kuanza kwa mkutano wa Tume hivi karibuni.

TSC YASIKILIZA NA KUAMUA RUFAA 49 ZA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Mruke (katikati), akibadilishana mawazo na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa, na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, wakati wa mkutano wa Tume hivi karibuni.



Baadhi ya wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakishiriki katika mkutano wa Tume hivi karibuni.

TSC YASIKILIZA NA KUAMUA RUFAA 49 ZA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Mruke (katikati), akibadilishana mawazo na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Bi. Bahati Mgongolwa, na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, wakati wa mkutano wa Tume hivi karibuni.



Baadhi ya wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakishiriki katika mkutano wa Tume hivi karibuni.

MAWASILIANO YANAYOZINGATIA TARATIBU, HURAHISISHA UTOAJI WA HUDUMA BORA

Na Mwandishi Wetu

Katika utumishi wa umma, namna jambo linavyowasilishwa ni muhimu kama jambo lenyewe. Ombi zuri likawasilishwa kwa njia isiyofaa linaweza kuchelewa kushughulikiwa. Malalamiko yenye msingi yakafikishwa katika ngazi isiyohusika yanaweza kuongeza usumbufu. Vivyo hivyo, taarifa inayopaswa kubaki ndani ya taasisi ikitolewa kwa mtu asiyehusika inaweza kumweka mtumishi katika mazingira ya kukiuka taratibu za utumishi.

Kwa mwalimu, anayefanya kazi katika mazingira yenye uhusiano wa karibu na wanafunzi, wazazi, jamii na Serikali, kuzijua na kuzifuata taratibu za mawasiliano si jambo la hiari. Ni sehemu ya uwajibikaji wa kiutumishi na maadili ya kazi.

Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya kazini ulioandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) unaeleza kuwa mawasiliano serikalini yanapaswa kufuata taratibu zinazolenga kuhakikisha uwazi, ufanisi na usalama wa taarifa. Mwongozo huo pia unasisitiza matumizi sahihi ya nyaraka rasmi, lugha yenye heshima, usiri wa taarifa na utoaji wa taarifa kwa umma na taasisi kupitia watu wenye mamlaka au waliokasimishwa kufanya hivyo.



Usipeleke jambo mahali pasipohusika
Miongoni mwa makosa yanayoweza kumletea mwalimu usumbufu ni kuwasilisha jambo katika ngazi isiyohusika au kuruka ngazi za kiutawala.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa TSC, mawasiliano ya watumishi kutoka ngazi za chini kwenda ngazi za juu yanapaswa kupitia kwa wasimamizi wa vituo vyao. Kwa mwalimu, mawasiliano hayo huanza kupitia kwa Mkuu wa Shule.

Hii ina maana kwamba mwalimu anapokuwa na ombi, hoja, changamoto au jambo linalohitaji uamuzi wa kiutawala, hatua ya kwanza siyo kutafuta njia ya moja kwa moja ya kumfikia kiongozi wa ngazi ya juu. Hatua ya kwanza ni kujua mamlaka inayohusika na kufuata mtiririko uliowekwa.

Kufuata mtiririko huo siyo kikwazo cha kupata huduma. Kinyume chake, ni njia ya kuweka jambo katika mikono ya mamlaka inayohusika na kulifanya liweze kushughulikiwa kwa utaratibu.



Barua siyo karatasi tu; ni kumbukumbu rasmi

Katika utumishi wa umma, mawasiliano ya maandishi yana umuhimu mkubwa kwa sababu huweka kumbukumbu ya jambo lililowasilishwa, tarehe lilipowasilishwa na hatua zilizochukuliwa.

Ndiyo maana mwalimu anapowasilisha ombi au jambo rasmi anatakiwa kuhakikisha kuwa nyaraka yake imeandaliwa kwa mtindo unaokubalika, taarifa ni sahihi, lugha ni rasmi na nyaraka muhimu zimeambatishwa.

Mwongozo wa huo unasisitiza kuwa nyaraka za Serikali zinapaswa kuandikwa kwa kuzingatia viwango maalumu vya uandishi, matumizi sahihi ya lugha, mpangilio wa nyaraka na usahihi wa taarifa.

Kwa hiyo, kabla ya kuwasilisha

barua, mwalimu anaweza kujiuliza maswali machache: Ninawasilisha kwa mamlaka gani? Ombi langu limeelezwa kwa uwazi? Nimeambatanisha vielelezo vinavyohitajika? Taarifa nilizoweka ni sahihi? Nimefuata njia inayotakiwa? Maswali haya yanaweza kuokoa muda mwingi baadaye.



Usichanganye mawasiliano rasmi na mawasiliano ya kawaida

Teknolojia imefanya mawasiliano kuwa rahisi. Simu, barua pepe na mitandao ya kijamii vinawezesha ujumbe kufika kwa haraka. Hata hivyo, urahisi wa kutuma ujumbe hauondoi wajibu wa kuzingatia taratibu za utumishi.

Kanuni na miongozo ya Serikali inatambua njia mbalimbali za mawasiliano, zikiwemo maandishi, simu na mawasiliano ya kielektroniki. Hata hivyo, matumizi ya mitandao ya kijamii katika mawasiliano ya taasisi yanapaswa kuzingatia idhini na mamlaka husika.

Hivyo, mwalimu anapaswa kutambua tofauti kati ya kutumia WhatsApp kumjulisha mwenzake jambo la kawaida na kutumia kundi la WhatsApp kusambaza taarifa rasmi ya Serikali au kutoa taarifa ambayo hauna mamlaka ya kuitoa.

Si kila taarifa uliyonayo kazini ni taarifa ya kusambaza.

Linda taarifa za Serikali

Mwalimu anaweza kukutana na taarifa mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi zinaweza kuwa za kawaida, lakini nyingine zinaweza kuwa na usiri au kuwa na matumizi maalumu ya kiutawala.

Mwongozo unasisitiza kuwa watumishi wa umma wanapaswa

MAWASILIANO YANAYOZINGATIA TARATIBU, HURAHISISHA UTOAJI WA HUDUMA BORA



kuheshimu usiri wa taarifa za Serikali na kuhakikisha kuwa hazitolewi kwa watu wasiohusika. Aidha, taarifa zinazotolewa kwa umma zinapaswa kuwa sahihi, wazi na zinazoeleweka, na zitolewe na watu wenye mamlaka au waliokasimishwa kufanya hivyo.

Hivyo, mwalimu anapaswa kuwa mwangalifu na kuepuka usambazaji wa taarifa usiokubalika ikiwemo kupiga picha nyaraka za ofisi na kuzisambaza, kutuma taarifa za kiutumishi katika makundi yasiyohusika au kutoa taarifa kwa vyombo vya habari bila kupata kibali cha mamlaka husika.



Malalamiko yana haki yake na yana utaratibu wake

Kuwa mtumishi hakumaanishi

kwamba mwalimu hana haki ya kulalamika au kuhoji huduma ambayo haridhishwi nayo. Kinyume chake, mfumo wa Serikali unatambua umuhimu wa kusikiliza na kushughulikia malalamiko ya watumishi.

Lakini hata malalamiko yana taratibu zake.

Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya kazini unaeleza kuwa malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa njia mbalimbali, zikiwemo maandishi, simu, kuonana ana kwa ana na njia za kielektroniki kama mifumo, barua pepe na tovuti.

Jambo muhimu ni kwamba mwalimu anatakiwa kutumia njia inayotambulika na kufuata utaratibu uliowekwa badala ya kugeuza malalamiko kuwa mabishano, matusi, vitisho au usambazaji wa taarifa katika mitandao ya kijamii.

Malalamiko yanapaswa kuwa njia ya kutafuta suluhisho, siyo chanzo cha tatizo jipya.

Tatizo lako linaweza kuwa halali, lakini njia yako ikawa siyo sahihi

Inawezekana kabisa kuwa mwalimu ana hoja ya msingi. Anaweza kuwa hajapata huduma kwa wakati, anaweza kuwa na changamoto kuhusu haki au stahili yake, au anaweza kuwa haridhishwi na uamuzi fulani.

Lakini uhalali wa hoja hauondoi wajibu wa kufuata utaratibu.

Kwa hiyo, mwalimu mwenye changamoto anapaswa kuanza kwa kujua tatizo ni la aina gani, mamlaka inayohusika ni ipi, njia gani inapaswa kutumika na ni vielelezo gani vinahitajika.

Hii inaweza kuifanya hoja yake ishughulikiwe kwa ufanisi zaidi.

Mawasiliano siyo ruhusa ya kuvuka mipaka ya kiutumishi

Wakati mwingine mtu anaweza kudhani kuwa kwa sababu ana haki ya kuwasiliana, basi anaweza kuwasiliana kwa namna yoyote na mtu yeyote. Si hivyo.

Mawasiliano ya mtumishi wa

umma yanaongozwa na wajibu wa kuheshimu mamlaka, kulinda taarifa, kutumia lugha inayofaa na kufuata taratibu zilizowekwa.

Mwongozo wa TSC unaonya kwamba matumizi mabaya ya mawasiliano yanaweza kusababisha taharuki, migogoro na mifarakano katika maeneo ya kazi. Pia unasisitiza kuwa taarifa za taasisi zisitolewe kwa watu wasiohusika na mawasiliano nje ya taasisi yafanywe na Mkuu wa Taasisi au mtu aliyekasimishwa.

Kwa mwalimu, hii ni muhimu hasa katika zama ambazo ujumbe unaweza kusambaa kwa watu wengi ndani ya sekunde chache.

Fanya mawasiliano kuwa daraja, siyo kikwazo

Lengo la taratibu za mawasiliano siyo kumzuia mwalimu kupata huduma. Lengo ni kuweka utaratibu unaofanya mawasiliano yawe na mwelekeo, uwajibikaji na kumbukumbu.

Mwalimu anayefuata utaratibu anarahisisha kazi ya anayepokea ombi lake, anaongeza uwezekano wa jambo lake kufikishwa katika mamlaka sahihi na kupunguza uwezekano wa kuchelewa kwa huduma kwa sababu ya makosa ya kiutaratibu.

Vilevile, mwalimu anayezingatia taratibu anajilinda dhidi ya kuingia katika mazingira yanayoweza kutafsiriwa kama utovu wa nidhamu, matumizi mabaya ya taarifa, kutoheshimu mamlaka au kukiuka maelekezo ya Serikali.

Ujumbe kwa mwalimu

Kufuata taratibu za mawasiliano siyo urasimu unaolenga kumzuia mwalimu kupata haki au huduma. Ni sehemu ya mfumo wa utumishi unaolenga kuhakikisha kuwa kila jambo linafikishwa katika mamlaka sahihi, kwa njia sahihi na kwa wakati unaofaa. Mwalimu anapofuata utaratibu, anajilinda, anaheshimu mfumo na anawezesha huduma kutolewa kwa ufanisi zaidi.

MAONESHU YA NANENANE 2026



Wateja waliotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye maonesho ya Nanenane 2026 wakiendelea kupatiwa huduma.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu